

JAMUHURI YA TANZANIA

KWAZI, MAWAZIRI, MAWAZIRI WADOGO, WAKUU WA MIKOA NA
WILAYA (REGIONAL COMMISSIONERS NA AREA COMMISSIONERS),
WAALIMU WOTE, NA WATUMISHI WA SERIKALI WOTE.

LUGHA YA KISWAHILI

Serikali inao wajibu mkubwa wa kukuza lugha ya Kiswahili. Ni jambo la muhimu kwa kila afisa na watumishi na viongozi katika taifa hili kutambua sawa wajibu huu na kutafuta kuutililiza, kwa kila njia iwezekanayo.

Hatua ya kwanza kabisa ipasayo kuchukuliwa ni kwa kila afisa na viongozi wenyewe kupata ujuzi mkubwa wa Kiswahili na kukisema barabara. Hivi tunakabiliwa na wajibu wa kuendeleza sana usemaji wetu sisi wenyewe wa lugha hii yetu tukufu ya Kiswahili. Unyonge mkubwa uliopo wa wanaelimu, maafisa, na viongozi wengineo, katika nchi yetu, ni kule kushindwa sana kujieleza kwa ufasaha katika Kiswahili. Unyonge huu hauna budi kuondolewa kwa haraka. Tabia mbaya sana ya kuchanganyachanganya Kiswahili na Kiingereza ni lazima iachwe.

Mgeni wetu mmoja ambaye pia alikuwa mtu maarufu alipata kusema maneno yafuatayo ambayo yana maana kubwa:— "Ikiwa lugha unayotumia ni ya kigeni, unakuwa kama mtu aliye katika nyumba ya mtu mwingine, bali ukiwa na lugha yako mwenyewe basi unakuwa kama mtu anayeishi katika nyumba yake mwenyewe".

Katika kukuza Kiswahili, si nia yetu kupuuza majifunzo ya Kiingereza. Kiingereza ni lugha ya dunia, na dunia inaendelea sana kuwa kitu kimoja. Basi ingekuwa jambo la kijinga sana kupunguza mkazo wetu wa kufundisha na kusema Kiingereza safi. Neno letu ni kuwa sasa budi Kiswahili nacho kifundishwe na kusemwa kwa ustadi sana kwani ndiyo lugha ya taifa. Kinakuzwa haraka kwa matazamio kwamba upesi iwezekanavyo (hatuwezi kujua ni wakati gani halisi) kazi zetu zote na za kila namna zitaendeshwa kwa Kiswahili.


Hivi basi tunamtaka kila afisa wa Serikali, na Viongozi wote, wawe mfano mwema katika kutumia lugha ya Kiswahili. Ikiwa ni kusema Kiswahili, kusemwe kwa usafi, ufasaha na utamu. Ikiwa ni kusema Kiingereza, basi hali kadhalika. Kusiwe na kuchanganyachanganya kule kunakoharibu sana lugha hizo mbili ambazo zinahitilafiana kabisa katika misingi yake ya namna ya kuwaza na jinsi ya kusema.

Huko baadaye itabidi watumishi wa serikali kutimiza ujuzi wa Kiswahili kiasi fulani wanapofikiriwa kupandishwa cheo. Itamfaa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa ujuzi wake wa Kiswahili unatosha kabisa kwa maendeleo yake katika kazi.

Nikiangalia mbele yetu zaidi sina budi kuwakumbusha maafisa wa elimu na waalimu wote kuwa ni wajibu wao kuona kuwa watoto na vijana wa shule zote wanakielewa sana Kiswahili. Basi wao wenyewe waalimu wakifahamu sana ikiwa watafundisha vizuri. Naomba wakuu wa shule waliwekee jambo hili macho makali.

Kiswahili kinaanza kutambulika na pahali pengi duniani kama lugha kubwa na ya maana. Katika Afrika ni Kiswahili peke yake kinachomtukua mtu mweusi kwa upande wa utamaduni wa lugha.

Wote tuone fahari katika lugha yetu ya Kiswahili.



R. M. KAWAWA, M.P.,
Makamu wa pili wa Rais